

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA HAMSINI NA TANO**

**28 JUNI, 2017**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

**KIKAO CHA HAMSINI NA TANO – TAREHE 28 JUNI, 2017**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari (Mb) na Shauri la Kusema Uongo Bungeni linalomhusu Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza (Mb).

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**452. MHESHIMIWA MGENI JADI KADIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mradi wa MIVARF ni wa Muungano na Makao yake Makuu yapo Arusha ambapo kazi yake kuu ni kujenga

masoko, miundombinu ya barabara, kuongeza thamani na kupeleka maendeleo Vijijini:-

Je, ni kwa kiasi gani mradi huu umechangia kuleta maendeleo Zanzibar.

### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **453. MHESHIMIWA DKT. DALALY PETER KAFUMU (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kutokana na Wananchi wa Vijijini kuwa na uelewa mdogo wa masuala ya Sheria na Haki zao, Watendaji wa Vijiji na wa Kata wakishirikiana na Mahakama za Mwanzo na Mabaraza ya Ardhi huwaonea na kuwadhulumu kwa kuwabambikizia kesi na kuwanyang'anya ardhi:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za kukomesha tabia hiyo.

#### **454. MHESHIMIWA MOSHI SULEIMAN KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Tangu mradi wa maji katika Kijiji cha Ngomalusa ukamilike haujawahi kutoa maji hata kidogo:-

Je, ni sababu zipi zilizofanya mradi huo usitoe maji kama ilivyokusudiwa.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**455. MHESHIMIWA DKT. PUDENCIANA WILFRED KIKWEMBE (KAVUU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Hitaji la kuni limekuwa kubwa kwa matumizi kama nishati ya kupikia na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira:-

Je, Serikali itawezesha vipi Wananchi kupata nishati mbadala kwa matumizi ya kupikia majumbani.

**456. MHESHIMIWA MENDRAD LUTENGANO KIGOLA (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Mtambula, Idunda, Itandula, Kiyowela, Idete, Maduma na Nyololo Shuleni.



## **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

### **457. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Mara kwa mara Serikali imekuwa ikishindwa kesi mbalimbali Mahakamani:-

Je, Serikali imefanya uchunguzi na kujua sababu za kushindwa kesi mara kwa mara.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **458. MHESHIMIWA HAMIDU HASSAN BOBALI (MCHINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kumekuwa na maswali yaliyokosa majibu stahiki kila mara kuhusu suala la mabaki ya Mjusi (*Dinosaur*) yaliyopo Ujerumani kila linapoulizwa au kuchangiwa hapa Bungeni:-

(a) Je, ni nini kauli ya mwisho ya Serikali kuhusu faida ambayo Wananchi wa Mkoa wa Lindi na Tanzania kwa ujumla watanufaika kutokana na mabaki hayo;

(b) Je, kwa nini Serikali isishauriane na Serikali ya Ujerumani kuboresha barabara na huduma za maji katika Kijiji cha Manyangara katika


Kitongoji cha Namapwiya ambapo mabaki ya Mjusi huyo yalichukuliwa.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **459. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itatatua au kumaliza kabisa tatizo la baadhi ya wakazi wanaoitwa Wahamiaji katika Vijiji vya Nyabuzume, Tiring'ati, Nyaburundi na Bigegu ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakisumbuliwa na hoja hiyo bila kupewa ufumbuzi.



## **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

### **460. MHESHIMIWA SALOME WYCLIFFE MAKAMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Zaidi ya kaya 800 za Wananchi wa mitaa ya Bukondamoyo na Mhunguala katika Kata ya Mhunguala Jimbo la Kahama Mjini wamezuiliwa kupatiwa huduma muhimu za kijamii kwa madai kwamba wanaishi kando ya Bwawa la

Nyihogo ilihali Wananchi hao wanaishi umbali wa zaidi ya mita 700 kutoka katika Bwawa hilo:-

Je, ni kwa nini Serikali inawanyima Wananchi hao huduma za kijamii wakati wako umbali wa mita 60 zilizowekwa kisheria.

**461. MHESHIMIWA ENG. ATASHASTA JUSTUS NDITIYE (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kwa muda mrefu sasa Mji wa Kibondo hauna maji baada ya chanzo cha maji kuharibiwa na shughuli za kibinadamu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mradi mwingine wa maji toka chanzo kingine (hasa Mto Malagarasi) ili Kata za Busunzu, Busagara, Lusohoko, Kitahana, Kumwambu, Kibondo Mjini na Miserezo zipate maji safi na salama.

**IV. HOJA ZA KAMATI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari (Mb) na Shauri la Kusema Uongo Bungeni linalomhusu Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza (Mb).



**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**MAAZIMIO:**

**WAZIRI MKUU:**

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation (ILO) – Maritime Labour Convention, 2006*).

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa Mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation (ILO) – Seafarers' Identity Documents Convention (Revised), 2003*).

**DODOMA**  
**28 JUNI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH**  
**KATIBU WA BUNGE**